

## 9A-Lahnul-Jaliy - Makosa (Makubwa) Ya Dhahiri

### 1. لحن الجلي Lahnul-Jaliy - Makosa (Makubwa) Ya Dhahiri

Makosa haya kama jina lake linavyoashiria ni kuwa yako wazi; kwa maana kuwa ni makosa makubwa ambayo wakati mwengine yanaharibu na kubadilisha maana iliyokusudiwa kwa uwazi kabisa; hivyo basi kila msomaji wa Qur-aan huweza kwa namna moja au nyengine kuwa ni mwenye kutumbukia katika makosa kama haya ambayo hubadilisha kabisa maana; iwe ya neno au Aayah nzima. Hukmu yake ni kuwa msomaji hupata dhambi kwa kuyafanya makosa haya ikiwa kwa makusudi.

Makosa haya hupatikana katika moja ya hali zifuatazo:

#### i. Makosa katika Makhaarij Al-Huruwf (Matokeo ya herufi) na Swifaatil-Huruwf (Sifa za herufi)

Kutamka makosa nako ni kuzitamka herufi za Qur-aan kutoka katika makhraj (matokeo) yasiyokuwa yake au kuipa herufi Swiffah isiyokuwa yake; kama ه badala ya خ, au ث badala ya س, au ك badala ya ق, au س badala ya ص, au ز badala ya ذ. Makosa kama haya kunapelekea kulifanya neno liwe na maana nyengine, maana ambayo ni tofauti kabisa na maana inayotakiwa kuthibitishwa katika Qur-aan.

Mfano wa kwanza:

قُلْ يَتَّيِبُوا الْكٰفِرُوْنَ ﴿١﴾

*Qul yaa ayyuhal-kaafiruwun ... .. ((Sema: Enyi makafiri!))<sup>1</sup>*

Kubadilisha herufi ya ق na badala yake kuitamka kama inavyotamkwa ك katika neno la: قُلْ

---

<sup>1</sup>Al-Kaafiruwun (109: 1)

Ukilitamka neno قُلْ (qul) kwa kuipa Swiffah zinazostahiki herufi ya ك (utatamka كُنْ 'kul') jambo ambalo litakupelekea kulitamka ق kama ni ك; na kwa kufanya hivyo tu utakuwa umefanya kosa lililo dhahiri na umebadilisha maana iliyokusudiwa na kulifanya neno liwe na maana nyengine “Kula enyi Makafiri” ambayo ni tofauti kabisa na maana iliyotakiwa hapo.

**Mfano wa pili:**

لَا يَلْفِ قُرَيْشٍ ۖ إِيَّاهُمْ رِحْلَةَ الشِّتَاءِ وَالصَّيْفِ ﴿٢﴾

... *rihlatash-shitaai wasw-swayf* ((Kwa ada ya Maquraysh)) ((Ada yao ya misafara ya majira ya baridi na majira ya joto))<sup>2</sup>

Kuibadilisha herufi ya ص na badala yake kuitamka kama inavyotamkwa س katika neno وَالصَّيْفِ

Ukilitamka neno وَالصَّيْفِ (*wasw-swayf*) lenye maana ya ‘majira ya joto’ kwa kuipa Swiffah zinazostahiki herufi ya س jambo ambalo litakupelekea kuitamka kama ni الصَّيْفِ (as-sayf); na kwa kufanya hivyo tu utakuwa umebadilisha maana iliyokusudiwa na kulifanya neno liwe na maana nyengine “.....na majira ya upanga” maana ambayo ni tofauti kabisa na maana iliyotakiwa hapo.

**Mfano wa tatu:**

ثُمَّ فِي سِلْسِلَةٍ ذَرْعُهَا سَبْعُونَ ذِرَاعًا فَاسْأَلْهُهُ ﴿٣﴾

... *sab-'uwna dhiraa'an faslukuwh* (“Kisha katika minyororo yenye urefu wa dhiraa sabiini muingizieni [mfunganisheni]”).<sup>3</sup>

Kuibadilisha herufi ya ذ na badala yake kuitamka kama inavyotamkwa ز katika neno ذِرَاعًا

<sup>2</sup>Al-Quraysh (106: 1-2)

<sup>3</sup>Al-Haaqah (69 : 32)

Ukilitamka neno lenye maana ya ذِرَاعاً (dhiraa'an) kwa kuipa Swiffah zinazostahiki herufi ya ز litakupelekea kuitamka kama ni زِرَاعاً (ziraa'an) utakuwa umebadilisha maana yake na kulifanya neno liwe na maana nyengine ".....minyororo yenye urefu wa ukulima sabiini..." maana ambayo ni tofauti kabisa na maana inayotakiwa kuthibitishwa.

**ii. Makosa katika kuzidisha neno au maneno:**

Mfano: kuongeza وَمَا فِي katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ

*"maa fis-samaawati wal-ardhw"<sup>4</sup>*

na badala yake ukatamka *"maa fis-samawaati wa maa fil-ardhw.*

**iii. Makosa katika kupunguza neno au maneno:**

Mfano: kuondosha لَنْ 'lan' katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

قُلْ إِنِّي لَنْ يُجِيرَنِي

*'qul inniy lan yujiyraniy<sup>5</sup>*

na badala yake ukatamka *'qul inniy yujiyraniy'.*

**iv. Makosa katika kubadilisha herufi ya neno:**

Kuweka herufi ya فَ badala ya و au و badala ya ف mfano katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

فَأَمَّا مَنْ أُوتِيَ

---

<sup>4</sup> An-Nuwr (24: 64)

<sup>5</sup> Al-Jinn (72: 22)

*“fa ammaa man uwotiya”*<sup>6</sup>

na badala yake ukatamka: *‘wa ammaa’* ukawa hukuitamka herufi ya ف

v. **Makosa katika kuthibitisha i’raab**<sup>7</sup>

Kuthibitisha *i’raab* (fat-hah, kasrah, dhwammah) katika neno au herufi ambayo sio yake mfano: kutamka fat-hah badala ya kasrah au badala ya dhwammah; au kutamka kasrah badala ya fat-hah au badala ya dhwammah; au kutamka dhwammah badala ya fat-hah na badala ya kasrah, au kuweka sukuwun shemu yenye *i’raab* au kuweka *i’raab* sehemu yenye sukuwn.

Ni makosa ya kawaida ambayo hutokezea mara kwa mara aidha kwa kuteleza ulimi au kwa kutokujua maana, isipokuwa kwa wale wenye ujuzi wa kuifahamu Qur-aan pamoja na ujuzi wa kanuni za *nahw* na *swarf*.<sup>8</sup> Ni mfumo wa alama zake za *raf-’u*<sup>9</sup>, *naswb*<sup>10</sup>, kama vile, nani mtenda na hutakiwa awe na *i’raab* gani, au nani mtendwa na hutakiwa awe na *’iraab* gani. Pia inapotangulia حرف جر *harfu jarr* (vihusishi) hubadilika *’iraab* ya neno linalofuatia kuwa ni yenye kasrah na kadhalika. Hivyo kuitia herufi *i’raab* isiyoistahiki kunaweza kupelekea kubadilisha kabisa maana ya Aayah nzima; kwani wakati mwengine hupelekea makosa kama haya kupotosha maana inayotakiwa kuthibitishwa, Mifano ifuatayo inafafanua.

**Mfano wa kwanza:**

إِنَّمَا تَخْشَى اللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ الْعُلَمَاءُ

*Innamaa yakhsha-Allaaha min 'ibaadihil-'Ulamaa*

<sup>6</sup> Al-Inshiqaaq (84: 7)

<sup>7</sup> Vokali: fat-hah, kasrah, dhwammah (kama a e i u)

<sup>8</sup> Nahau na sarufi katika lugha ya Kiarabu.

<sup>9</sup> Dhwammah

<sup>10</sup> Fat-hah

**((Hakika wanaomkhofu Allaah [kikweli kweli] miongoni mwa waja Wake ni 'Ulamaa.))<sup>11</sup>**

Kosa likitendeka katika Aayah hii humteremsha Allaah daraja Yake na kumfanya Yeye ni mja na mja kuwa ndio Mola, jambo ambalo ni hatari kubwa na dhambi. Ni kosa la kutahadhari nalo.

*I'raab* inayotakiwa kuthibitishwa juu ya herufi ya ه ni fat-hah<sup>12</sup> katika tamshi la *Lafdhwul-Jalaalah* الله kwa kuwa hapa inatakiwa isomwe: الله'

(Allaaha') kwa kuithibitisha fat-hah juu ya ه yenye kuonesha kuwa الله

Ndiye mtendwa (*maf-'uwl*) Ndiye anayeogopwa. Na maana hii haitoweza kupatikana na kueleweka isipokuwa kwa kuithibitisha hiyo fat-hah na ndio maana iliyokusudiwa kuwa "**Wanaomkhofu Allaah** (سبحانه وتعالى) .....". Lakini ukilisoma tamshi la الله (Allaahu') kwa kulipachika *i'raab* ya dhwammah<sup>13</sup> badala ya fat-hah utakuwa umebadilisha maana kabisa na kupotosha kwa kumfanya Mtendwa الله kuwa ni mtenda (*al-faa'il*), Ambaye ni muhali kwake kuwa na sifa kuogopa. hivyo basi umepotosha kwa kuifanya Aayah ithibitisha maana nyengine: "**Kwa hakika Allaah Ndiye Mwenye kuwakhofu Maulamaa**"! Maana hii hakuna aneikubali katika wenye kumwamini Allaah na Siku ya Mwisho kwani inathibitisha lililo muhali kwa Allaah.

**Mfano wa pili**

✽ وَإِذْ أَيْتَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ رَبُّهُ بِكَلِمَاتٍ فَأَتَمَّهُنَّ ۗ

***Wa idhibtalaa Ibraahiyma ...***

**((Na [taja] Alipojaribiwa Ibraahiym na Mola wake kwa maneno, naye akazitimiza))<sup>14</sup>**

*I'raab* inayotakiwa kuthibitishwa juu ya herufi ya م ni fat-hah kwa kuwa hapa inatakiwa isomwe: إِبْرَاهِيمَ (Ibraahiyma) kwa kuithibitisha

<sup>11</sup> Faatwir (35: 28)

<sup>12</sup> *I'raab* inayoandikwa juu ya herufi za hati za kiarabu kuwakilisha vokali ya a.

<sup>13</sup> *I'raab* inayoandikwa juu ya herufi za hati za kiarabu kuwakilisha vokali ya u.

<sup>14</sup> Al-Baqarah (2: 124)

fat-hah juu ya مَ yenye kuonesha kuwa Ibraahiyma ndiye mtendwa (*maf-'uwl*) ndiye aliyejaribiwa. Na maana hii haitoweza kupatikana na kueleweka isipokuwa kwa kuithibitisha hiyo fat-hah na ndiyo maana iliyokusudiwa kuwa “Allaah Alimjaribu kwa kumpa mtihani Ibraahiym”. Lakini ukilisoma tamshi إِبْرَاهِيمَ (Ibraahiymu) kwa kulipachika *i'raab* ya dhwammah badala ya fat-hah utakuwa umebadilisha maana kabisa na kupotosha, kwa kumfanya Mtenda اللهُ kuwa ni mtendwa (*maf-'uwlun-bih*), , Ambaye ni muhali kwake kuwa na sifa ya kufanyiwa mitihani na viumbe Vyake wakiwemo Mitume (عليهم السلام), hivyo basi umepotosha kwa kuifanya Aayah ithibitisha maana nyengine: “Na Ibraahiym alipomjaribu Mola wake...”! Maana hii hakuna anayeikubali katika wenye kuamini Allaah na Siku ya Mwisho kwani inathibitisha lililo muhali kwa Allaah.

**Mfano wa tatu:**

فَعَصَى فِرْعَوْنُ الرَّسُولَ فَأَخَذْنَاهُ أَخْذًا وَبِيلاً

*Fa'aswaa Fir'awnur-Rasuwla ...*

**(([Lakini] Fir'awn alimuasi (huyo) Rasuli, Tukamchukuwa mchukuo wa kuangamiza))<sup>15</sup>**

*I'raab* inayotakiwa kuthibitishwa juu ya herufi ya ن ni dhwammah kwa kuwa hapa inatakiwa isomwe: فِرْعَوْنُ (Fir-'awnu) kwa kuithibitisha dhwammah juu ن yenye kuonyesha kuwa Fir-'awnu ndiye mtenda (faa'il), ndiye aliyeasi.

Ama kuhusu neno الرَّسُولَ (Ar-Rasuwla) *'iraab* inayotakiwa kuithibitisha juu ya herufi ya ل ni fat-hah kwa kuwa hapa inatakiwa isomwe: الرَّسُولَ (ar-Rasuwla) kwa kuithibitisha fat-hah juu ya ل yenye kuonesha kuwa Ar-Rasuwla ndiye mtendwa (*maf-'uwl*) ndiye

<sup>15</sup>Al-Muzzammil (73 :16)

aliyeasiwa; na maana hii haitoweza kupatikana na kueleweka isipokuwa kwa kuithibitisha hiyo fat-hah juu ya herufi ya ج.

Makosa hayo yatakapotendeka kuipa ن fat-hah na kuipa ج dhwammah hubadilisha kabisa maana na kufahamika kuwa “Mtume alimuasi Fir-a’wn”; maana inayopotosha kabisa ambayo hakuna anayeikubali katika wenye kuamini Allaah na Siku ya Mwisho kwani ni tofauti kabisa na maana inayothibitishwa na Qur-aan

vi. Makosa katika مَدُّ الطَّبِيعِي Maddutw-Twabiy’iy<sup>16</sup>

Kosa hili ni lenye kutendwa na wengi wasiofahamu hukmu za Tajwiyd; kutamka neno kwa kutokuvuta harakah mbili inapokuwa ina مَدُّ الطَّبِيعِي (maddutw-twabiy’iy) au kulitamka neno kwa kuivuta zaidi ya harakah mbili, japokuwa halina chenye sababu ya kulivuta.

**Mfano wa kutokuvuta herufi:**

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿١٦﴾

*Innaa Nahnu Nazzalnaa-dhikra ...*

**((Hakika Sisi Tumeteremsha dhikri [Qur-aan] na hakika Sisi bila shaka ndio Tutakaoihifadhi [isibadilishwe kwa vyovyote]))<sup>17</sup>**

Herufi ya اِنَّا katika neno إِنَّا (innaa) inatakiwa ithibitishiwe *ghunnah* na *swiffah* ya *shaddah* (kukazwa) kisha inatakiwa ivutwe harakah mbili katika kusomwa kwake ili lilete maana yake iliyokusudiwa kuwa “**Hakika Sisi**”. Ama lisipovutwa na ikasomwa (inna) itamaanisha “**Hakika**” bila ya kuweko kiwakilishi (*dhawmiyr*) cha “**Sisi**”.

**Mfano wa kuvuta herufi:**

إِنَّ الْأَبْرَارَ لَفِي نَعِيمٍ ﴿١٧﴾

<sup>16</sup> Madd ya kimaumbile au ya asili

<sup>17</sup> Al-Hijr (15 : 9)

## *Innal-abraara lafiy Na'iyim*

**((Hakika Al-Abraar [watendao mema] bila shaka [watakuwa] katika neema.))<sup>18</sup>**

Herufi ya ى katika neno اِنَّ (inna) inatakiwa ithibitishiwe *ghunnah* na Swiffah ya *shaddah* (kukazwa) lakini haitakiwi ivutwe harakah mbili kama zinavovutwa herufi zenye madd, kwani hapa haistahiki kuvutwa ili ilete maana iliyokusudiwa kuwa ni: “**Hakika**”. Hivyo basi msomaji akiivuta herufi ya ى hapa kwa haraka mbili, huwa ameengeza herufi na hubadilika na kuwa اِنا (inna) yenye kubeba maana tofauti na ile iliyotakiwa kuthibitishwa na kwa kuisoma hivyo huwa na maana “**Hakika Sisi**”.

### vii. Makosa ya kukaza neno (Shaddah) au kutokukaza

Kuacha kukaza herufi inayostahiki kukazwa (shaddah) au kutamka herufi kwa kukaza isiyostahiki kukazwa.

#### a) Mfano wa kutokukaza herufi inayostahiki kukazwa:

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ أَبَىٰ وَاسْتَكْبَرَ وَكَانَ مِنَ

الْكٰفِرِيْنَ ﴿١٤﴾

*Wa idh Qulnaa lil Malaai-katis-sjuduw li-Aadama fasajaduw illaa ibliysa abaa ...*

**((Na [taja] Tulipowaambia Malaika: “Msujudieni Aadam.” Wakasujudu isipokuwa Ibliys alikataa...))<sup>19</sup>**

Neno اِلا (illaa) hapa linastahiki kukazwa kwa kuwa lina shaddah, na huwa na maana kuwa ‘isipokuwa’, na wakati wowote ule lisipokazwa katika kulitamka kwa kuiondosha shaddah juu ya herufi

<sup>18</sup>Al-Infitwaar (82 :13)

<sup>19</sup>Al-Baqarah (2: 34)



ya ٱ atakuwa mtu amelisoma إِلَى (*ilaa*) ambayo italeta maana ya 'kuelekea kwa' badala ya 'isipokuwa': na maana ya Aayah nzima itabadilika na kuwa "Na [taja] Tulipowaambia Malaika: "Msujudieni Adam." (Malaika wote) wakamsujudia Ibliys...". Hivyo itakuwa msomaji amempachika cheo na kumvisha kilemba cha ukoka Ibliys laana ya Allaah iwe juu yake kwa kumaanisha kuwa kasujudiwa na Malaika, na hili ni muhali wala hakuna katika wenye kuamini Allaah na Siku ya Mwisho wenye kukubali hilo.

**b) Mfano wa kukaza herufi isiyostahiki kukazwa:**

Kukaza herufi ya ر katika neno la رَبُّكَ ukaitamka "*wa marrabbuka*" badala ya "*wamaa Rabbuka*" katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى)

وَمَا رَبُّكَ بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيدِ

*"wa maa Rabbuka...."*